HABARI ZA DIVISHENI YA AFRIKA MASHARIKI NA KATI NA MFANO WA KUVUTIA

CONNECT

JANUARI – MACHI
2020



Kipaumbele Cha Utume

Jengo Kubwa la Matumizi mbalimbali lafunguliwa AUA...Uk.10

Kanisa la Waadventista Ethiopia lapangwa upya kwa utume... Uk. 14

Taarifa Mpya za Mgogoro wa Burundi...Uk. 13

Kipaumbele Cha Utume Mwaka 2020



Mada ya “Kipaumbele cha Utume: Ni Wakati wa Mavuno!” haihusu kujaribu kuwafanya watu waishi katika hali ya afya, au kujenga tabia zao na kupanga kwa namna inayorandana na mwongozo wa Maandiko ulio dhahiri. Ingekuwa kazi ya kanisa ni kufanya tabia za watu zifuate viwango au kanuni zilizokubaliwa, pasingekuwa na umuhimu wa kweli kwa sababu Biblia inasema kwamba hata matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi.
Bila kukataa thamani ya viwango na kanuni za Imani, ule mfano wa mwizi msalabani unatuambia kwamba kuna umuhimu wa kipaumbele cha utume ambacho kinazidi mambo mengine yote. Watu halisi wanakufa kimwili na kiroho bila kuwa na matumaini yanayoweza kupatikana katika Kristo pekee.

Siku ya kuamkia mwaka mpya nilikutana na mwanamke anayeitwa Nellie akiwa amekata tamaa ya kupata tumaini katika maisha yake mwaka uliokuwa unafuata, lakini pia hakuwa na uhakika kama alitakiwa kumkimbilia Kristo au kumkimbia. Alieleza matukio ya kusikitisha yenye maumivu katika maisha yake, na jitihada zake za kutafuta nafuu kutoka katika ulimwengu wake wa mateso ambazo hazikuzaa matunda. Kipaumbele cha muhimu cha Natallie na mamilioni wengine (pamoja na baadhi yetu tulio kanisani) siyo kujifunza mtindo mpya wa maisha, bali ni kupata maisha mapya katika Kristo. Kwa kweli hatuwezi kupata mtindo mpya wa maisha hadi hapo tutakapopata kwanza maisha kupitia kwake yeye (Yohana 15:5)

Ninamheshimu sana Nellie. Yeye alikuwa na akili ya kutosha kufahamu kwamba kuna kitu hakikuwa sawa katika maisha yake, na kwamba hakuogopa kubadilika. Inaonekana kuwa jambo pekee alilokuwa akiogopa, lilikuwa ni hali ya kukata tamaa hapo atakapojaribu kurudi tena kujipatia matumaini. Hakuwa tayari kabisa kukubali kubadilisha mtindo wake wa maisha. Alitaka, na kuona haja ya maisha mapya, na akahisi kwamba Mungu asingemwona kama mwenye kustahili kupata nafasi nyingine kama hiyo.

Pengine kadiri unavyosoma hapa unatambua kwamba umekubali tu mtindo wa maisha na kwamba unakosa nguvu na ari inayoweza kupatikana katika maisha mapya na uhusiano ambao ni Kristo pekee anayeweza kukupatia. Ikiwa hii ndiyo hali uliyo nayo, ninakualika ufanye dhana ya ‘kutafuta maisha mapya katika Kristo’ iwe ni kipaumbele chako cha utume mwaka 2020.

Kwa kweli kuwatafuta wana na binti kama Nellie waliopotea katika ulimwengu, ndicho kipaumbele cha utume wa Mungu mwaka huu mpya, na miaka mingine yote. Ni kipaumbele cha utume wa kanisa kwa sababu tunafahamu kwamba Baba yetu wa mbinguni mwenye upendo, anaumia wakati wote ambao watoto wake wanapotea bila Yeye katika ulimwengu huu. Nilimwambia Nellie kwamba, Mungu bado anamtaka katika maisha yake bila kujali kiasi ambacho ameshindwa katika maisha. Tafadhali tumwombee.

Utume ni kipaumbele chetu kwa sababu ni kipaumbele cha Mungu. Anatamani kuunganika na watoto wake ambao hawaonekani. Wamedanganywa na kuibiwa kutoka kwake, na hivyo anataka wote wamrudie. Tunaomba kwamba mwaka huu uwe ni mwaka wa kuvuna kwa ajili ya Kristo na kwa ajili ya mamilioni wanaofanana na Nellie. Hicho ndicho Kipaumbele cha Utume: Ni Wakati wa Mavuno!

Emanuel Pelote
Mhariri wa CONNECT

Picha ya Jalada: Sifa zimwendee David Pelote

CONNECT (ISSN 0777-001X) Jan – Mar 2020 Gombo la 5. Namba 1. CONNECT huchapishwa kwa robo, mara nne kwa mwaka na Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati ya Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato, 0053 Sanduku la Barua Binafsi Mbagathi, Nairobi, Kenya. Ni bure kwa washiriki wa kanisa la ECD. ©2020 Kanisa la Waadventista wa Sabato Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati. Kando ya hapo, picha na taswira zote ni sehemu ya picha zilizohifadhiwa. Adventist® na Seventh-day Adventist® ni alama za biashara za Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato zilizosajiliwa. Wasiliana nasi kupitia barua pepe hii: connect@ecdadventist.org au simu namba +254-733-333-373

Seventh-day Adventist® Church

DIVISHENI YA AFRIKA MASHARIKI NA KATI
www.ecdadventist.org

Rais
Blasious Ruguri

Katibu
Alain Coralie

Mhazini
Jerome Habimana

Mkurugenzi wa Mawasiliano
Prince Bahati

Wafanyakazi wa CONNECT

Mhariri wa CONNECT
Emanuel Pelote

Misioni ya Unioni ya Congo Mashariki
Elkanah Kerosi

Misioni ya Union ya Ethiopia Mashariki
Ato Mihret Dagnew

Union Konferensi ya Mashariki ya Kenya
Catherine Nyameino

Misioni ya Unioni ya Kaskazini Mashariki ya Congo
Martin Mayenze

Union Konferensi ya Tanzania Kaskazini
Daniel Bulengela

Misioni ya Union ya Rwanda
Onesphore Yadusoneye

Himaya Shikizi ya Sudan Kusini
John Taban

Misioni ya Union ya Tanzania Kusini
Christopher Ungani

Misioni ya Union ya Uganda
Immanuel Ogwal

Misioni ya Union ya Congo Magharibi
Albert Biselele

Misioni ya Union ya Ethiopia Magharibi
Abdisa Tirfesa

Union Konferensi ya Kenya Magharibi
Philip Gai

Msanii
Diane I. Kibuuka

Mtafsiri – Kiswahili
Moseti Chacha

Gombo la 5. Namba 1

HABARI ZA DIVISHENI YA AFRIKA MASHARIKI NA KATI NA MFANO WA KUVUTIA

CONNECT



Nguvu Ya Kuwashirikisha Waumini (TMI)

Tangu awali, Mungu ametufundisha kwamba, kuwa pamoja ni sehemu muhimu ya mpango wake kwa ubinadamu. Alitaka tupate uzoefu unaofanana na ule wa Baba, Yesu na Roho wanaopitia uzoefu pamoja. Ni hiyo hali ya kuwa pamoja, wakiunganishwa na upendo ambao matokeo yake ni nguvu ya Mungu isiyopimika. Na nguvu hiyo hiyo ndiyo inayokuwa kwetu tunapoungana pamoja naye kwa upendo.

Hii ndiyo siri iliyofanya jitihada zetu za Kuwahusisha Washiriki Wote (TMI) zikaweza kugusa maisha ya wengi kiasi hicho. Tunapounganika pamoja, nguvu tuanayokuwa nayo ni kubwa kuliko kama wote tungekuwa tunamtumikia Mungu lakini kila mmoja kwa namna na wakati wake. Nguvu ya Roho wa Mungu inazidisha kila kitu tunachofanya pamoja kwa Jina lake. Jambo maalum kuhusu ECD, ni ile hali ya kuwa familia ambayo imejifunza kuinuka juu ya mambo yale ambayo yangeweza kutugawanya tunapomtumikia Mungu katika utume. Hakuna jambo la muhimu kuliko hilo. Inakuwa na mantiki. Hata hivyo, ndivyo ilivyoanza.

Mungu hakutaka mwanadamu awe peke yake katika bustani ya Edeni ili wapate kumtukuza na kumtumikia pamoja. Haikutosha kwa Mungu kwamba Abraham awe peke yake akimtumikia. Badala yake, Mungu alikusudia kwamba Abraham aanzishe jamii mpya ya watu ambao wangemwabudu Muumba pamoja. Katika kitabu cha Matendo ya Mitume sura ya 2, tunawaona mitume wakisubiri kwa pamoja ahadi ya Mungu. Na wakati wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali, ndipo kukaja ghafula toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Hiyo nguvu ndiyo iliyoanza mapinduzi na uamsho ambao hadi leo bado unabadilisha ulimwengu!

Nguvu ya Kuwahusisha Washiriki Wote (TMI) haimaanishi kwamba tukija pamoja itaongezeka au kuzidishwa. Bali nguvu ya Mungu ndani yetu inaongezeka upendo unaporuhusiwa kutuleta pamoja. Tunapopendana, tunafanana naye zaidi kadiri tunavyofanya kazi kwa ajili ya ufalme. Ninaamini kwamba ndiyo maana Yesu mara nyingi alitusihi tupendane sisi kwa sisi. Ndiyo maana alitusihi tusameheane kila mmoja na mwenziwe, na kujitoa kwa unyenyekevu kila mtu kwa mwenzake. Huu ni mpango wa Mungu. Ndiyo maana simba wanatembea pamoja. Tunaliona hili katika swala ambao wanatembea pamoja, tunaliona pia katika makundi ya tembo, katika ndege wa angani na hata katika samaki majini. Wanakuwa na nguvu wanapokuwa pamoja. Kwa hiyo tuendelee kuinuka juu ya huu mgawanyiko wa kidunia. Juu ya utaifa na ukabila. Juu ya lugha na tamaduni. Tumebarikiwa kuwa na waumini wapya zaidi ya milioni 1.5 tangu tumeanza mahubiri ya Kuwahusisha Washiriki Wote (TMI) zaidi ya miaka 4 iliyopita. Mungu ameonesha nguvu zake kwa kutusaidia. Hebu Mungu na atubariki zaidi na zaidi kadiri tunavyomaliza kazi, tukipigana huku tukiwa na nguvu ya Mungu kwa ajili ya ufalme wake. Pamoja.

Daktari Blasious Ruguri ni Rais wa Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati ya Kanisa la Waadventista wa Sabato

Je, Mtindo wenye afya ni Kipaumbele Cha Utume?



Ingawaje mtindo wa maisha una maana nyingi, Makala hii itafafanua mtindo wa maisha kama njia ya maisha. Mtindo wa maisha wenye afya unapunguza hatari ya kuugua na kuzidi, au kufariki mapema. Pia unazidisha uwezekano wa kuzuia au kucheleweshe magonjwa yanayoathiri afya kama yale ya moyo.

Lishe bora kama Kipaumbele cha Utume

Virutubisho vinayotokana na chakula tunachokula vinalisha na kujenga mwili wako. Pia ni lishe, ulinzi na namna ya kurudishia chembe hai mpya. Lishe inayokosekana kwenye chakula chako ni ukosefu katika mwili wako. Hivi viashiria hasi baada ya muda vinajenga hali ya mtindo wa maisha ulio dhaifu. Kwa hiyo basi, mtindo wa maisha wenye afya unadai lishe bora. Ndiyo maana ni muhimu kuchunguza kwa makini chakula chako! Hicho chakula kina virutubisho gani? Je, kile unachokula kinategemeza utendaji wote wa chembe hai mbalimbali na ustawi wako?

Mazoezi ya Kimwili kama Kipaumbele cha Utume

Chembechembe hai za miili yetu, ambazo zinajenga sehemu mbalimbali za miili yetu, na viungo tofauti vinavyofanya kazi kwa pamoja kwa namna ya upatanifu, kila chembe hai ikifahamu umuhimu wake na umuhimu wa chembe hai zingine, zilisanifiwa kujongea, kujongea, kujongea, kujongea! Chembechembe hai zingine zinaungana kutengeneza, wakati zingine zinajongea kuvunja. Chembe hai zingine zimepewa kazi ya kusafirisha, zingine kuondoa sumu, kupigana, kuunda na kusafisha. Kuna maelfu na maelfu ya utendaji tofauti ukiendelea kila sekunde kwa kujiendesha bila kuleta mkanganyiko wowote. Chembechembe hai hizi zinakuwa na utendaji hafifu mazoezi yanapokosa. Mazoezi ya mara kwa mara ya kimwili yanaimarisha kila chembechembe hai ili ifanye kazi katika kiwango stahiki.

Afya ya Akili kama Kipaumbele cha Utume

Msongo ni namna mwili unavyojibu mabadiliko yoyote yanayohitaji marekebisho au mwitikio. Kujizuia kuchukua hatua mabadiliko yanapohitajika kunasababisha makovu na vurumai. Baadhi ya mambo yanayoweza kusaidia kuboresha afya ya akili ni kuwa na mwelekeo chanya kwa matumaini, ukiwa na mtazamo mwema. Kumbuka kwamba hakuna hali yoyote inayodumu. Halafu, kubali hali ambayo wewe mwenyewe hauwezi kuibadilisha wala kuitawala. Tawala namna unavyotazama dunia inayokuzunguka kwa fikira chanya.



“miili ... makao bora ya Roho Mtakatifu.

Hali ya kujiona sehemu ya jamii inaboresha afya na furaha. Ule ukaribu na wengine unaondoa upweke na kukuza stadi na uimara. Tenga muda wa kuwa peke yako na Mungu. Tenga muda wa kuwa na familia, marafiki, na jumuia inayokuzunguka. Jifunze kutoa. Fanya kazi za kusaidia. Jitolee kufanya kazi mwenyewe au katika vikundi katika jumuia yako au katika mashirika ya misaada yanayoshughulika na watoto yatima, wazee, wanyama na mazingira. Maisha yanakuwa bora unapokuwa ukigusa maisha ya wengine.



Mapumziko kama Kipaumbele cha Utume

Miili yetu inahitaji mfumo sahihi wa kulala na kupumzika. Kufanya hivi kunarejesha ujana na kuponya bongo zetu, huku ukirekebisha utendaji wa mfumo wetu wa ndani na kuponya mwili wetu. Tunapokiuka hii mizunguko ya asili katika miili yetu, tunakaribisha magonjwa na misongo. Saa iliyoko ndani ya mwili wetu inatawala usingizi, joto la mwili, utendaji wa ndani ya mwili na kuachia vichocheo mwilini. Maana yake ni kwamba tunahitaji kudumisha ratiba elekezi iliyo bora ya ulaji, kupumzika na kulala inayosimamiwa kikamilifu. Faida kubwa ya ratiba inasimamiwa vyema ni kwamba tutaweza kufanya kazi kwa namna iliyo bora zaidi, na kuwa wazalishaji wazuri tunapokuwa na afya.



Kiasi katika mambo yote kama Kipaumbele cha Utume

Kitu chochote kisichoweza kutawaliwa, kinamfanya mhusika kuwa mtumwa wa hicho kitu. Uraibu wa vitu kama pombe na hata vitu kama chai na kahawa umedai na kumiliki hali ya kujitawala ya watu wengi, ukiwanyang’anya uhuru, afya na furaha. Uraibu unaweza kuwa ni wa chakula, madawa ya kulevya, simu, na kadhalika. Mtindo mzuri wenye afya hautakiwi kumfanya mtu kuwa mtumwa kwa mpangilio wa mwenendo ambao mhusika hawezi kuutawala.

Sababu za Mwenendo wenye Afya kama Kipaumbele cha Utume

Chaguzi zetu zilizo nzuri, zitatufanya tujisikie vizuri na kuonekana vizuri. Mwisho wake mwonekano wetu utajitokeza na kuhubiri bila maneno, na Mungu atatukuzwa.

Mtindo wa maisha wenye afya katika maisha ya waumini utafanya miili yao kuwa makao bora ya Roho Mtakatifu.

Mwili wa Kristo unaweza tu kutamka “Enendeni ulimwengu” pale unapoweza kuingia mahali ambapo panaweza kuingilika na ujumbe wa afya kupitia kwa mtu fulani anayeuishi. Kwa namna pana, tumecheleweshe ujumbe huu kuwafikia wote kwa kukosa kuufanya kipaumbele katika misha yetu. Je, huu siyo wakati muafaka wa kufanya afya zetu zilizo nzuri kuwa kipaumbele cha utume wetu? Ombea jambo hili sasa hivi, kisha chukua hatua moja kwa wakati leo.

Hesperance Deodate ni Mtaalamu wa Lishe kutoka Tanzania

Kila mahali kuna mwelekeo wa kubadilisha kazi ya shirika iwe ni jitihada za mtu binafsi. Hekima ya kibinadamu inaokena kujikusanya pamoja, kujielekeza mahali pamoja, katika kujenga makanisa makubwa na taasisi. Wengi wanaachia taasisi na mashirika kazi ya ukarimu; wanatoa udhuru kwamba hawawezi kugusana na ulimwengu, na kwa kufanya hivi, mioyo yao inapoa. Hatimaye wanakuwa wabinafsi wakijiangalia wenyewe bila kujali wengine. Upendo wao kwa Mungu na kwa wanadamu unakufa nafisini mwao. Yesu ameweka kwa wafuasi wake kazi ya kila mtu mmoja mmoja kufanya – kazi ambayo haiwezi kufanyika kwa uwakilishi. Huduma kwa wagonjwa na masikini, kufikisha injili kwa waliopotea, haitakiwi kuachwa mikononi mwa kamati au vitengo vya misaada vilivyobuniwa. Wajibu binafsi, jitihada binafsi, kujitoa mhanga kwa kila mmoja binafsi, ndilo hitaji la injili – ***The Ministry of Healing, uk. 147; ChS 10.2***

Mungu anataka kila mmoja awe mtendakazi katika shamba lake la mizabibu. Unatakiwa kufanya kazi uliyopewa kusimamia na kuifanya kwa uaminifu. The Bible Echo, June 10, 1901 (The Review and Herald, May 1, 1888. ChS 9.4

Kama maisha ya kila mmoja yangekuwa ni misionari ulio hai, ujumbe wa wakati huu ungetangazwa kwa haraka katika nchi zote, na kwa watu wote, mataifa yote, na lugha zote. Testimonies for the Church, 6:428. ChS 9.5

Kila mwanafunzi wa kweli amezaliwa katika ufalme wa Mungu kama mmisionari. Ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujikia uzima wa milele. Yule anayepokea anageuka na kuwa mtoaji. Neema ya Kristo katika nafsi ni kama chemchemi jangwani, ikibubujisha na kuwahuisha wote, na kuwafanya wale ambao wanakaribia kuangamia watake kunywa haya maji ya uzima. ***Desire of Ages, uk. 195. ChS 9.6***

Mungu anatazamia huduma binafsi kutoka kwa kila mmoja aliyekabidhiwa elimu ya ukweli wa wakati huu. Siyo wote wanaoweza kwenda kama wamisionari katika nchi za kigeni, lakini wote wanaweza kuwa wamisionari katika maeneo mahalia kwenye familia zao na katika ujirani. Testimonies for the Church, 9:30 ChS 9.7

Yesu alikuwa amesimama hatua chache tu kutoka katika kiti cha enzi cha mbinguni alipowaagiza wanafunzi wake. Hawa ni pamoja na wamisionari wote ambao wataamini katika jina lake, alisema kuwa: “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Katika agizo hili, ilikuwa nguvu za Mungu ziandamane nao. ***The Southern Watchman,*** September 20, 1904 ***(The Review and Herald, October 6, 1896). ChS 9.8***

Kila mmoja anayemkiri Kristo anatakiwa kufanya kazi ya kuokoa roho kuwa ni kazi ya maisha yake yote. Sisi ni wadeni wa ulimwengu kwa neema tuliyopewa na Mungu, kwa ile nuru iliyoangaza kwetu, na kwa uzuri huu uliogunduliwa na nguvu ya ukweli. Testimonies for the Church 4:53. ChS 10.1

Ellen G. White (1827-1915) ni mmoja wa waanzilishi wa kanisa la Waadventista wa Sabato na aliandika kwa kina akitoa utambuzi wa kiroho kutoka katika Biblia kwa jumuia ya Imani katika uwanda mpana wa mada.





TMI 2.0 Hali Ya Usoni ya Uinjilisti Katika ECD

SWALI: Katika kipindi hiki cha miaka mitano ya kalenda ya utawala ya kanisa la Waadventista wa Sabato, washiriki wa ECD wameongezeka kwa takriban milioni 1.5. Je, unadhani kigezo muhimu kilichochangia katika matokeo bora ya uinjilisti hapa ni kipi?

JIBU: Tumegundua kwamba Imani ya Kikristo imekubali kosa la msingi ambalo limeathiri utume wetu. Tumefanya uinjilisti wetu uwe wa kitaalam ili washiriki wote waamini kwamba kabla ya kufanya uinjilisti, ni lazima uwe mchungaji, ni lazima uwe na elimu ya shahada baada ya miaka mingi ya kujifunza haya mambo kwenye seminari mahali fulani. Katika uzoefu wa mitume, baada ya Stefano kupigwa mawe na mateso kuanza, Biblia inasema katika kitabu cha Matendo ya Mitume 8:4 kwamba siyo makuhani wala mitume peke yao, bali ilikuwa ni wale watu wa kawaida walioitwa walei, walioongolewa, na waliokuwa na uzoefu na Yesu, ndio waliopeleka Injili ulimwenguni kote. Kwa hiyo basi, jambo la muhimu tulilofanya ni kukataa dhana potovu na tukashawishi wengi wa washiriki wetu kwamba uinjilisti ni sehemu ya mtindo wa maisha inayotarajiwa kwa kila mshiriki aliye katika Imani.


SWALI: Ni nini kinachohitajika ili uwe mwinjilisti?

JIBU: Ni lazima Yesu awe halisi kwako. Hauwezi kushiri kile usichokuwa nacho. Mshiriki yeyote ambaye ameongoka kwa dhati hatahitaji kuambiwa awe mwinjilisti kwa sababu uinjilisti kimsingi ni ushuhuda wa kile ambacho Bwana amekutendea. Wengi wa washiriki wetu wamejenga uhusiano na mafundisho yetu, lakini wanapungua kwa kukosa kujenga uhusiano halisi na Yesu Kristo. Mafundisho yanasaidia pale tu mtu anapokuwa ameongoka kwa kukutana na Yesu. Katika kitabu cha Yohana sura ya 9 tunamwona mtu aliyezaliwa akiwa kipofu, akianza kushiriki na wegine kile ambacho Mungu alikuwa amemtendea baada ya kuponywa na Yesu. Mwanamke Msamaria aliweza kuleta mji mzima kukutana na Yesu kwa sababu alitaka wafahamu kuhusu hili tumaini jipya ambalo alikuwa amepewa na Yesu. Elimu inaweza kuwa na manufaa, na wengine wameitwa kujifunza ili kuipata hiyo elimu, lakini jambo moja ambalo ni la muhimu ni kuongolewa na Yesu na kuwa na Roho wake Mtakatifu ndani yako. Kwa hiyo sasa, tunataka kuhakikisha kwamba kila mshiriki, hata watoto wetu, hata wale washiriki ambao hawana elimu iliyo rasmi, wanajihusisha katika uinjilisti. Mungu haangalii uso wa mtu. Kwa hiyo kile tunachotaka ni kuhakikisha kwamba kila mshiriki wa familia ya kanisa la Waadventista wa Sabato ni mwanafunzi aliyeongoka, ambaye anashiriki na wengine kile ambacho Mungu amemtendea.

SWALI: Kuna nguvu hapo. Vigezo muhimu vya TMI 2.0 ni vipi?

JIBU: Kuna vipengele vitatu. Kwanza kuna Kuongoa Roho, hapa kila mshiriki anashiriki ushuhuda wake na wale wasio washiriki kuhusu kile ambacho Bwana amemtendea. Kisha kuna kulea, pale ambapo waumini wanashiriki kile ambacho Mungu anamtendea kila mmoja wao, ili kwamba waweze kushirikiana mizigo kila mmoja na mwezake na kutiana moyo. Jambo la mwisho kuna kutangaza, pale tunapowatafuta kwa makusudi kabisa wale ambao adui ameiba kutoka katika familia yetu. Wakati mwingine hakuna neema ya kutosha katika jumuia zetu. Ukikosea kidogo tu, mara nyingi inaonekana kuwa hakuna neema kanisani kwa ajili yako. Lakini Biblia haifundishi kwamba usharika wa waumini uwe wa namna hiyo. Kwa hiyo tunataka kuhakikisha kwamba tunarejesha washiriki wa zamani na kuwsaidia kushinda majaribu yao ili kwamba sisi sote tuweze kusihi maisha ya ushindi pamoja.

Daktari Joel Okindo ni Mkurugenzi wa Uinjilisti na Msaidizi wa Rais wa Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati.



Kipaumbele cha Mungu

Ni Nini?

Utume wa kanisa la Waadventista wa Sabato ni kufanya wanafunzi wa Yesu Kristo, kutangaza injli ya milele iliyo katika ujumbe wa malaika watatu, na kutayarisha ulimwengu kwa ajili ya kuja kwa Kristo kulikokaribia. (Mathayo 28:18-20 Matendo 1:8; Ufunuo 14:6-12).
Kutokana na tamko hilo tunapata kipaumbele, na umuhimu wa utume wa Kristo na agizo lake kwa kila muumini katika Kristo. Yesu akiwaagiza wanafunzi wake, aliwaamuru kwenda toka pale walipokuwa hadi miisho ya dunia, na kufanya wanafunzi katika kila taifa wakiwabatiza na kuwafundisha. (Mathayo 28:18-20 Matendo 1:8).

Yesu mwenyewe alituonesha maana ya kufanya wanafunzi. Mwisho wa utume wake hapa duniani, aliwafanya wale aliokuwa nao wahitimu kutoka katika kuwa wanafunzi hadi kuwa mitume kwa kuwatuma kwenda na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi akiwapatia mchakato wa kuwazidisha ambao ungejirudufu hata mwisho wa dunia.
Kitabu cha Ufunuo kinasisitiza umuhimu wa agizo hili pale kinapozungumza kuhusu ujumbe wa malaika watatu. Katika sura ya 14, tunasoma kwamba anaonekana malaika mwingine, “akiruka katikati ya mbingu akiruka katikati ya mbingu, mwenye Injili ya milele, awahubiri hao wakaao juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji.” (Ufunuo 14:6-7)
Hizi jumbe za malaika watatu zinadhihirisha kipaumbele cha utume wa Mungu katika ulimwengu wakati huu ulio muhimu sana katika historia ya dunia hii. Umuhimu na asili ya umakinifu wa jumbe zake unadhihirisha uharaka na asili ya umakinifu wa utume ambao Yesu aliwapatia wanafunzi wake.
Yesu mwenyewe anasema kuwa, “Imetupasa kuzifanya kazi zake yeye aliyenipeleka maadamu ni mchana, usiku waja asipoweza mtu kufanya kazi.”(Yohana 9:4) Kwa namna iyo hiyo, Kristo anatazamia mwili wake, ambao ni kanisa lake, kujihusisha kupitia katika Neno lake, vitendo na maombi, katika kazi ya kuokoa wenye dhambi ambao hawana matumaini leo kama sisi tulivyokuwa hapo awali. Hili ndilo linalotakiwa kuwa tamanio letu kuu na jambo la kujishughulisha nalo, kwa sababu Biblia inaonesha kwamba kwa namna iliyo dhahiri hili ni suala la Mungu. Utume wa malaika watatu unatuonesha hili.
Ni kweli kwamba Mungu anataka kuokoa ulimwengu aliouumba. Hiki kwa kweli ndicho kipaumbele cha utume wake. Lakini pia ndicho kipaumbele cha utume wake, kukamilisha ukombozi wake kupitia kwetu sisi ambao ametuita ili kufanya wanafunzi. Anataka kuufikia ulimwengu wote. Na anataka kufanya hivi kupitia kwetu.

Mara kutakapokuwa na matokeo sahihi kupitia katika kukabiliana na Mwalimu Mkuu wa kimbingu (Isaya 6:4-8), hakuna mwenye dhambi atakayeweza kuzuia habari njema za wokovu wake mwenyewe. Tutaruka dhidi ya mambo yasiyokuwa sawa kama yule kipofu na kuuambia ulimwengu kuwa, “Najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sasa naona.” (Yohana 9:25), kwa utukufu wa Bwana. Katika kujishughulisha kwetu kote katika tasnia na ajira, Kristo anategemea kwamba tuwe “chumvi ya ulimwengu” na “nuru ya ulimwengu” (Mathayo 5:13-16) kadiri tunavyovuta na kugusa wengine kuja kwa Mungu. Familia zetu na uhusiano wetu vinatakiwa kuzama na karama ya upendo (Wagalatia 5:22-23) kutoka ndani yetu kwenda kwa kila mmoja wetu. Katika kupanga familia, kanisa, sehemu ya kazi, au jumuia, upendo wa Mungu ulioko ndani yetu unatakiwa kuonekana katika namna tunavyoishi na kudhihirishwa kama barua iliyo wazi ikisomwa na watu wote. (2 Wakorintho 3:2)

Kipaumbele cha utume kinampatia changamoto kila mmoja aliyeongoka, familia na kanisa lililo hai, kuleta mguso katika mazingira yao kwa shuhuda zilizo hai za vitendo vya kuokoa vya Bwana kupitia katika maneno na matendo yao.

Moses Maka Ndimukika, PhD Mkurugenzi na Mkuu wa Chuo Kikuu cha Bugema, Kampala.



Jinsi nilivyopata Kipaumbele changu cha Utume

Inaonekana kuwa kwa watu wengine, kuweka malengo na kupanga mipango ni zoezi gumu, au ni changamoto isiyowezekana. Sivyo ilivyo kwangu. Tangu nikiwa mtoto, nilikuwa nikisikia sauti zikiniambia kuwa, “Usijilinganishe na Jones.” Kila nilipoondoka nyumbani kwa shughuli za siku hiyo, nilikumbushwa kwa upole kuwa, “Siku zote kumbuka kwamba wewe ni mtoto wa nani.” Nilikuwa nimeweka kiwango cha elimu nilichokusudia kufikia kama utume wangu maishani. Nilifahamu fika kwamba, elimu ndiyo inayoweza kumwinua mtu bila kujali hali aliyo nayo. Elimu ilifanya lengo lolote kufikiwa, kama tu lingekuwa ndani ya upeo wetu wa kifedha.

Nilifikiri kamba lengo langu maishani ilikuwa ni kupata elimu nzuri na hatimaye kufanikiwa. Nikiwa msichana mdogo tu, nilitambua kwamba kupata elimu nzuri ni muhimu kwa ajili ya siku zangu za usoni, kama ilivyo kwangu kukuza sifa pambanuzi za tabia kama vile huruma, uaminifu, heshima, uadilifu, na kujiamini. Elimu nzuri pamoja na mazingira ya nyumbani yenye ustawi viliniwezesha kukuza uelewa mwema wa mazingira yangu kiulimwengu. Naamini kwamba hata mbingu zingenipokea kama wengine wote walioonesha ujasiri wa kuifikia hiyo mbingu walivyopokewa. Nilifikiri kwamba elimu ilikuwa ni jibu la matatizo ya maisha ya kila mtu, kwa hiyo nilisoma majarida ya *Reader’s Digest, National Geographic, Strength and Health*, na kusikiliza idhaa za BBC na zingine za nyumbani zote zilizoweza kunihabarisha.

Lakini mwelekeo wangu katika elimu, pamoja na maadili havikuniambia chochote kumhusu Mungu wala kunionesha mahali pangu kwake. Kulingana na marehemu baba yangu, huduma kwa ubinadamu, kutokuwa na ubinafsi, na kuridhika zingekuwa ni funguo za kufungua moyo wa Mungu. Kwa kutumia hayo yote kwa msukumo wa dhati, nilifikia mahali ambapo nilifanikiwa kukamilisha malengo yote niliyoweka tangu utoto hadi chuo kikuu. Malengo yangu yote shuleni hadi ngazi ya chuo kikuu yalifikiwa. Lakini kifo cha baba yangu kilinoa mwelekeo wangu zaidi kwa mambo ambayo hayawezi kukamilishwa kupitia katika jitihada binafsi. Nilianza kumwomba Mungu ambaye sikuwa namfahamu sana. Pamoja na kuomba, nilianza kufunga pia na kudai ahadi zilizopo katika Biblia, ndipo nikapata majibu yaliyonipa uhakika.

Baadaye mume wangu aliponieleza kuhusu semina ya ‘Ufunuo wa Kweli za Ajabu’ aliyokuwa amehudhuria, nilijenga shauku ya kina katika kujifunza Biblia, kuhusu Muumbaji, amri kumi, na kuhusu Mwokozi aliyefufuka. Utambuzi wa kimantiki ulikoma kuwa hitaji langu la mwisho. Badala yake nilitaka tu upendo wa Mungu, kumtumainia na kuwa na Imani kwake. Kadiri nilivyoendelea kujifunza kuhusu Kristo alivyofanyika mwili, kifo chake msalabani, kukubaliwa kwangu kama mrithi wa Mungu na kwamba ningekuwa mrithi pamoja na Kristo, ndivyo nilivyozidi kumpenda Yesu.

Kule kufahamu yale yote Yesu aliyonifanyia kumeondoa hofu ya mambo katika maisha haya na hofu ya hisia zozote za kushindwa kufikia viwango vya ulimwengu huu. Hofu iliyobaki kwangu ni uwezekano wa kurudi kusongwa na mahangaiko ya maisha ya kila siku nikitafuta namna ya kuifanikisha kesho ili nipate kuendelea kuishi, kiasi cha kupoteza ule ukaribu wa kutembea na Kristo nilio nao sasa. Mara nyingi nilikuwa na wasiwasi kuhusu kutafuta staha na thamani yangu katika kile nilichokuwa mimi mwenyewe. Sasa ninapata vitu vyote hivyo katika kile ambacho Kristo amefanya ndani yangu. Sasa nina Amani. Ndiyo maana kumfahamu Kristo kumekuwa kipaumbele change cha utume.

Daktari Yetunde Odeyemi ni mshauri kwa kitaalam wa ofisi ya jimbo la Afrika la ADRA







Chuo Kikuu cha Wadventista cha Afrika Kinafungua Jengo Kubwa la Matumizi Mbali Mbali

Chuo kikuu cha Waadventista cha Afrika (AUA) kilianza kusherehekea siku tatu za mwisho wa juma kuanzia tarehe 1 hadi 3 Novemba 2019 kwa ajili ya tukio kubwa la kufungua na kusimika jengo kubwa la matumizi mbali mbali kwa kumbukumbu ya Lindsay Thomas Jr., PhD. Jengo hili kubwa lililogharimu mamilioni ya fedha za kigeni limekusudiwa kuashiria enzi mpya yenye uwezo ulioongezeka na fursa kwa ajili ya chuo kikuu ambacho kwa sasa kinahifadhi ukumbi wa mikutao wa kisasa wenye teknolojia ya hali ya juu unaoweza kukalisha watu 1,200 kwa namna nzuri ukilinganisha na kumbi zingine zilizo bora zaidi katika taifa. Jengo hili kubwa ni muunganiko wa majengo manne pamoja yakiwa na ukumbi mmoja, maeneo ya kuegesha magari, jiko la kitaalam na bwalo, madarasa kadhaa yaliyo bora, na eneo la mikutano nje ya nyumba pamoja na maofisi.

Jengo hili kubwa lilipewa jina la marehemu Daktari Linday Thomas, PhD ambaye ni Wakili aliyekuwa na shauku ya elimu ya juu, mchungji mlei na mchangiaji wa muda mrefu wa Maendeleo ya Waafrika. Daktari Lindsay Thomas pamoja na mke wake Daktari Evelyan Thomas alifurahiwa sana kati ya wafadhili wengine wengi kwa namna alivyojitoa mhanga wakati wa sherehe za uzinduzi. Jengo hili limekuwa na sifa kubwa kwa ajili ya mambo yanayofanyika hapa pamoja na namna usanifu wake ulivyojali mazingira. Jengo hili la ukumbusho limejengwa katika viunga vya kilima cha Advent likiwa na kitengo kinachoelekea mashariki kikizama gorofa mbili chini ya usawa wa ardhi kwenye miamba ya mkoa wa Kajiado.

Mradi wa kuendeleza jumba hili la mikutano uliongozwa na Makamu wa Mwenyekiti wa AUA Daktari Delbert Baker na timu yake katika chuo kikuu wakipata usaidizi kamili wa Mkuu wa chuo cha AUA, Daktari Blasious Ruguri. Zaidi ya hapo katika kutoa huduma pana zaidi na utume kupitia katika chuo kikuu, moja ya malengo yaliyoratibiwa kwa mradi huo ilikuwa ni kuhakikisha kuwa jengo linakamilika bila kubakiza madeni kwa chuo kikuu. Shukurani za pekee zilitolewa kwa wafadhili wakati wa uzinduzi maalum wa jengo hilo kubwa kwa sababu ni wao, pamoja na neema na upendeleo wa Mungu, ndio waliowezesha lengo kubwa hilo kufikiwa.

Kuanza kwa mfululizo wa matukio kulitanguliwa na kupata jina la upande wa jengo ambalo hapo awali lilikuwa la utawala wa AUA na kuliita Bermpong na Mabel Owusu-Antwi. Tukio hili lenye maana lilitofanyika siku ya Ijumaa lilichukuliwa kama utangulizi wa sherehe za uzinduzi zilizofanyika Jumapili tarehe 3 Novemba. Daktari Brempong Owusu-Antwi ambaye ni Makamu wa Mwenyekiti mtangulizi wa chuo cha AUA, pamoja na mfuasi wake Daktari Delbert Baker, walifunua kitambaa kilichofunika jina la jengo la zamani la utawala mbele ya utawala wa AUA, kitivo, wafanyakazi wote na marafiki. Huduma ya kanisa yenye hamasa ilifanyika siku ya Jumamosi asubuhi kwa kushirikiana na viongozi wa juu wa ECD. Mhubiri ambaye ni mwimbaji mashuhuri anayefahamika duniani kwa jina la Wintley Phipps, alitoa hubiri lenye nguvu lililojawa na Roho kuhusu umuhimu wa kukua kwa Wakristo wakijenga tabia kama ya Kristo. Aliwatia moyo Wakristo kuiga tabia ya Kristo bila kuingiza mambo mengine wala kuihafifisha.

Mgeni Rasmi kwa ufunguzi huo, Profesa Magoha alizungumza na hadhira kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Kenya, Mheshimiwa Uhuru Kenyatta, akimpongeza taasisi kwa kukamilisha kwa mafanikio ujenzi wa jumba kubwa hilo kwa kushirikiana na wasaidizi wengi walioasaidia kuhakikisha njozi hiyo inakuwa halisi. Liwali wa jimbo, ndugu Ole Lenku alionesha kujivunia AUA na maendeleo yake hata uwezo wa kitaaluma unaochangiwa katika urithi wa utamaduni na viwango vya elimu katika jimbo la Kajiado na kwingine kote.

Baada ya kufikia tamati ya ufunguzi asubuhi ile, kipindi cha burudani kwa muziki kiliendelea katika jumba zuri hilo la mikutano jioni yake. Kwa kweli Mchungaji Phipps aliimba kwa ubora usiopimika siku hiyo ya Sabato mwishoni wimbo ule, *"Mungu Atukuzwe"* kwa mambo makuu aliyotenda.

Kwa taarifa zaidi kuhusu huduma inayotolewa hapa na program za elimu katika AUA tafadhali tembelea tovuti hii: www.aua.ac.ke

---

Janet Oyende ni Afisa Mahusiano wa Chuo Kikuu cha Waadventista cha Afrika.









Extravaganza Iliyofanyika Nakuru Katika Misioni ya Union Konferensi ya Mashariki Mwa Kenya

Maelfu ya washiriki wa kanisa, viongozi na wengine walifurahia kwaya, shuhuda, maonesho, mahubiri, na shughuli nyingine nyingi zilizofanyika katika extravaganza ya mwisho ya utume katika ngazi ya Union na kuandaliwa na Union ya Kenya Mashariki. Tukio hili lilifanyika tarehe za 1 hadi 7 Desemba kule Nakuru kwenye viwanja vya Chama cha Kilimo cha Kenya. Tukio hili lilitangazwa hewani mubashara kote katika nchi ya Kenya na pia kupitia katika mitandao na Hope Channel ya Kenya.

Ili kuonesha mada ya tukio hili, yaani “Kuokolewa kwa Neema”, vikundi mbalimbali viliingia katika kufanya usafi mitaani, kugawa nguo na vyakula, kutoa huduma za tiba bure na kugawa vitabu na vijuzuu, chini ya uogozi wa idara ya huduma za wanawake, idara ya huduma za afya ya Waadventista pamoja na huduma za uchapaji. Idara ya huduma za wanawake pia ilionesha Neema ya Mungu kwa mamia ya watoto wa mitaani kule Nakuru kwa kuwaogesha, kuwanyoa, kuwalisha na kuwavika.

Hizi jitihada zilikuwa ni uwakilishi stahiki wa Neema iliyozungumzwa na Daktari Alain Coralie, alipogusia kwenye hubiri lake ile neema ya kweli katika mtindo wa maisha ya Kikristo kama udhihirisho wa namna mtu anavyoweza kuakisi upendo wa Mungu. Daktari Coralie anaafiki kwamba kutunza tu baadhi ya sheria hakutoshi katika kuishi Kikristo.

Viongozi wa Divisheni ya Afrika ya Mashariki na Kati (ECD) walihudhuria, pamoja na baadhi ya vongozi wa divisheni zingine na watendakazi wa ngazi za juu kutoka union zingine kama vile Union ya Magharibi mwa Kenya na union zingine mbili kutoka Tanzania.

Wageni wanaowakilisha uongozi wa jumuia mahalia walikuwepo pia katika tukio hilo. Siku ya Sabato makamu wa liwali wa jimbo la Kericho Daktari Suzan Kikwai ambaye ni mdau mkubwa wa huduma za Waadventista na katibu wake Joel Bett waliungana na maelfu ya walioabudu katika viwanja hivyo. Mhazini wa jimbo hilo ndugu Domic Nyabuto, na Daktari Peter Kantyenya ambaye ni waziri wa Fedha na mipango ya uchumi kwa jimbo hilo pia alikuwapo.

Katika hotuba yake, Daktari Kentyenya alisifu kanisa la Waadventista wa Sabato kwa jukumu lao la kuendeleza ustawi wa kiroho na kijamii kwa washiriki wake na majirani. Wakati wakipokea mchango wa kiti cha kusukuma kutoka kwa timu ya uokoaji ya konferensi ya kati ya bonde la ufa, Daktari Kentyenya alisema kwamba serikali ya mahali hapo itaingia ubia na kanisa ili kuwasaidia watu kwa mahitaji yao maalum. Konferensi ya Union ya Kenya Mashariki pia ilitoa mchango wa mapipa kadhaa ya taka kwa jimbo hilo ili kusaidia kudumisha usafi wa mji wa Nakuru.

Mchungaji Daktari Balasious Ruguri katika hubiri lake siku ya Sabato, alikumbusha hadhira iliyokuwa imejumuika pale kwamba Mungu anatuita tutoke katika maeneo yetu ya faraja ya dhambi, anafanya kitu kipya katika maisha yetu. Mchungaji Ruguri alisema kwamba, Mungu kwanza anaondoa ile hali ya ubinafsi ndani ya watu ndipo awatayarishe kwa ajili ya wajibu mpya anaowapatia. Neema ya kuondoa mambo ya kale ndani ya mtu inafuatiwa na neema ya kumwita mtu na kumtayarisha ili kutimiza kusudi kubwa katika maisha. Akirejea katka kisa cha wito wa Abraham, Mchungaji Ruguri alisema kwamba ili mtu amtumikie Mungu kwa ubora zaidi ni lazima ang’olewe kutoka katika utamaduni wa awali na kutoka katika kila kitu kilichokuwa kinamzuia asiweze kuwa mhudumu katika wito mpya alioitwa.

Imeandaliwa na **Catherine Nyameino-Ontita**, Mkurugenzi wa Mawasiliano, EKUC



Mkutano wa Wachungaji na Wake za Wachungaji kule Tanzania

Mwezi wa Desemba 2019, Chama cha Huduma za Wachungaji na Huduma za Wake za Wachungaji wa Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati katika Halmashauri Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato (ECD) kiliratibu mkutano wa wachungaji na wake za wachungaji kule Singida, Tanzania maeneo ya Kanisa la Waadventista wa Sabato Kibaoni. Zaidi ya wachungaji 1,300 na wake zao walihudhuria kutoka katika union zote mbili za taifa hilo.

Katika mkutano huo, wake za wachungaji takribani 526 walipokea vyeti vya kufuzu kutoka katika mtaala maalum wa mafunzo ambao uliendeshwa kwao na Huduma ya wake za Wachungaji ya ECD. Wachungaji 32 pia waliwekewa mikono siku ya Sabato mchana. Sifa zilitolewa kwa Bwana kwa kubatizwa kwa watu wawili siku hiyo, mmoja wapo akiwa ni mchungaji wa dhehebu jingine aliyekuwa akijiunga na kanisa la Waadventista wa Sabato.
Wakati wote wa mikutano, kulikuwa na namna ya pekee ya kuwatambua wachungaji wastaafu waliotayarisha namna ya kukamilisha utume katika mazingira magumu sana. Wachungaji hao na wake zao walipewa tuzo za kutambua utendaji wao kama ishara ya shukurani na upendo kwa miaka mingi ya huduma ya uaminifu.

Jambo moja lililokaziwa juma hilo lilikuwa ni viapo maalum vya ndoa vilivyofanywa upya kwa wenzi walio katika huduma waliyohudhuria. Kwa kutambua umuhimu maalum wa ndoa za hao walioitwa kutumika katika huduma, ombi la pekee lilitolewa na wakatiwa moyo, wakiaswa kukataa kila aina ya vurugu na unyanyapaa lakini kukumbatia unyenyekevu na upendo ili kwamba Kristo aheshimiwe katika mahusiano yao.

Mkutano huo ulikuwa na utajiri wa uhuisho wa kiroho uliofanyika na mchungaji Jerry Page, ambaye ni Katibu wa Huduma za Kichungaji. Mchungaji Page alisisitiza kwa nguvu hitaji kubwa la wachungaji kuweka kipaumbele katika kukuza uhusiano binafsi na Mwokozi, uhusiano ule wanaouhubiri. Alishiriki visa binafsi vingi vinavyohusiana na mke wake Janet, ambaye hakuweza kuhudhuria mikutano kwa sababu ya tatizo la kiafya (ambalo kwa kweli Mungu ameshajibu kwa kumponya kutokana na maombi mengi). Pamoja na hayo, wachungaji na viongozi waliohudhuria walipata uzoefu wa ushawishi wa Roho kutaka kufanya dhana ya kumfahamu Kristo iwe ni kipaumbele chao cha kwanza katika huduma. Mkutano pia uliongozwa na Mama Audrey Folkenberg, ambaye alisafiri kutoka China kuja kuhudhuria mikutano hii na kuhudumu hasa kwa wake za wachungaji waliokuwa wamehudhuria. Mchungaji Emanuel Pelote ambaye ni msaidizi wa Mwenyekiti, alishiriki baadhi ya jumbe kwa wachungaji, akisisitiza nguvu ambayo inatoka kwa wachungaji wanaohudumu wakijikita kwenye uanafunzi binafsi wenye nguvu. Daktari Tsegaye Fesaha, mkurugenzi wa huduma za Afya alizungumza juu ya afya katika huduma. Mchungaji Musa Mitekaro ambaye ni Mkurugenzi wa Huduma za Kichungaji na Familia wa ECD pamoja na mkewe Mama Winfreda Mitekaro anayeongoza wake za wachungaji ECD, wakishirikiana na mumewe waliongoza shughuli zote katika tukio hilo. Walifanya hivyo wakisaidiwa kwa sehemu kubwa na wenzao katika idara hizo kutoka Tanzania ambao ni Mchungaji Herbert Nziku na Mchungaji Daniel Ndiegi, pia Mama Rache Mahende na Mama Frida Mika.

Wenyeviti wa union zote mbili za Tanzania, Daktari Godwin Lekundayo kutoka Union Konferensi ya Kaskazini mwa Tanzania na Mchungaji Mark Malekana kutoka Misioni ya Union ya Kusini mwa Tanzania walihusika kikamilifu katika tukio hilo, na hasa kwa sababu huu ulikuwa ni wakati muhimu sana kwani siyo mara nyingi kwamba wake za wachungaji wakutane pamoja kwa ibada wakitiana moyo kwa namna ambayo waume zao huwa wanafanya. Uwepo wa wake za wachungaji ulikuwa ni muhimu kwa mafanikio na nguvu ya mkutano. Mchungaji Mark Malekana alitumia muda huo kuwaomba wachungaji kuungana, kuachana na siasa kanisani, kuendelea kutafuta ushauri kutoka kwa wastaafu na kusonga mbele wakiuishi wito wao kutoka kwa Mungu.

Union mbili hizi za Tanzania zina wachungaji zaidi ya 750 kwa pamoja wakitumika katika shamba la mzabibu, wakihudumia takribani washiriki 500,000 walio Waadventista, na karibu milioni 56 wengine katika taifa hilo ambao bado hawajaupokea ukweli wa kurudi kwa Yesu ambako kuko karibu sana.

Daniel Bulengela ni Mzalishaji wa vipindi kutoka Hope Channel Tanzania

Taarifa Mpya Kuhusu Upeo wa Mgogoro wa Burundi



Lambert Ntiguma



Lameck Barishinga

Karidi tunavyoingia katika mwaka mpya, ni muhimu kuwakumbuka ndugu zetu na dada zetu wa Burundi ambao wamepitia katika mateso nchini kwao. Wengi wao wanaupokea mwaka mpya wakiwa nyuma ya kuta za magereza. Kwa hali yoyote waliyo nayo, hawatakabiliana na adha hiyo wakiwa peke yao kwa kuwa Kristo aliye Bwana ameahidi kuwa pamoja nao na kwamba hatawaacha kamwe. Familia katika Kristo pia hitashindwa kuendelea kuwakumbuka.

Mgogoro wa uhuru wa dini kule Burundi ulianza Novemba 2018 pale mwenyekiti mmoja mstaafu wa union moja alikataa kuondoka madarakani wakati majukumu yake yalipotakiwa kuchukuliwa na kamati kuu ya utendaji ya divisheni. Kwa kutumia nguvu za dola, huyu mwenyekiti alipewa mamlaka ya kuendelea kumiliki na kutawala ofisi za kanisa na miamala ya benki kinyume na sera za kanisa. Pamoja na kwamba alikuwa ametolewa katika uongozi kama mchungaji na kwamba asingeendelea kushikilia nafasi hiyo ya kanisa rasmi, mvuto aliokuwa nao kwa marafiki zake katika serikali uliendelea kuchochea mgogoro huo. Misingi ya Imani ya kanisa la Waadventista wa Sabato hairuhusu serikali kutawala utendaji wa misioni ya kanisa. Kwa sababu hii, kanisa limekosa uchaguzi katika jambo hili, ila kusisitiza katika haki iliyotolewa na Mungu ya kutenda kazi zake bila kuwa chini ya utawala wa serikali.

Bahati mbaya mateso haya katika kanisa la Waadventsta huko Burundi hayakuishia kwenye vitisho katika uhuru tu. Viongozi wa Waadventista na washiriki wamekabiliana na vitisho na hata kutishiwa usalama wao na uhuru. Baadhi ya washiriki wamenyanyaswa na kupigwa hata wakati mwingine huduma ya hospitali ililazimika kutafutwa. Hivi karibuni ECD waliachia video katika tovuti yao ikionesha viongozi wa vyombo vya usalama wakiwapiga na kuwanyanyasa Waadventista ambao walikuwa wanatafuta tu kumwabudu Mungu siku ya Sabato ndani ya kanisa lao. Taarifa kwamba zaidi ya washiriki 300 wametupwa magerezani kwa vipindi mbali mbali zimefikia ofisi za ECD Mchungaji Lameck Barishinga ambaye ndiye aliyeteuliwa rasmi na Misioni ya Union ya Burundi amewekwa katika gereza la Mpimba kwa zaidi ya miezi miwili. Imani yake kwa Mungu bado ni imara, na anaendelea kuomba tumweke katika maombi yeye mwenyewe pamoja na kanisa la Waadventista wa Sabato kule Burundi. Mwenyekiti wa Misioni ya Kusini Magharibi mwa Burundi Mchungaji Lambert Ntiguma paia amefungiwa rumande ya Polisi ya Jabe.

Mungu hajasahau washiriki wote wa Burundi na makanisa yao. Mwanzoni mwa Desemba, katika mkutano maalum wa wachugaji wote na wake zao kule Tanzania, wito wa pekee ulitolewa na wachungaji wote wakaombea wapendwa wanaoteseka kule Burundi. Siku maalum ya maombi na kufunga iliendeshwa katika divisheni ya Afrika Mashariki na Kati tarehe 16 Novemba 2019.

Mchungaji Ted Wilson ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Kanisa la Waadventista wa Sabato amekuwa akituma ujumbe wa kutia moyo mara kwa mara, ambao Mwenyekiti wa ECD, mchungaji Blasious Ruguri amekuwa akiwashirikisha waumini wa kanisa kule Burundi. Katika ujumbe wake wa hivi karibuni kwa washiriki wa Burundi, Mchungaji Ruguri aliwakumbusha kwamba hii siyo vita dhidi ya nyama na damu, na kwamba isije ikapiganwa kwa harakati na vurugu. Badala yake aliwakumbusha kwamba watu wa Mungu hupigana kwa kuwa waaminifu katika kumtii Kristo. Aliwaambia pia kwamba, “Sisi sote tunashawishika kwamba Mungu anafanya kazi ndani yenu kwa namna iliyo kubwa sasa kuliko alivyofanya hapo awali. Ninafahamu kwamba huu mgogoro utakapokoma, sote tutampa Mungu utukufu kwa muujiza huo na hapo tutakuwa tumejifunza kile alichokuwa akifanya kati yetu kwa kipindi chote hicho.”

Ni dhahiri kwamba washiriki wa Burundi wamekuwa wakiongezeka idadi kwa ushuhuda wa uaminifu kwa nguvu za Kristo. Taarifa za maendeleo ya mgogoro huo mara kwa mara kwa picha na video zinaweza kupatikana kwenye tovuti ya ECD, www.ecdadventist.org. Tafadhali kumbuka kuombea kanisa la Burundi.

Mchungaji Emanuel Pelote ni Mhariri wa Gazeti la “Connect” na Msaidizi wa Rais wa Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati

Mfumo wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Kule Ethiopia Kubadilishwa Kuwa Misioni





Misioni ya Union ya Ethiopia Mashariki - **Kwa mzunguko wa akrabu:** Tadesse Adugna (Rais), Petros Negash (Katibu) na Tihtina Bekele (Mhazini)





Misioni ya Union ya Ethiopia Magharibi - **Kwa mzunguko wa akrabu:** Geremew Biru (Rais), Belay Taye (Katibu) na Zemenu Zelalem (Mhazini)

Mwaka 2015, ECD iliandaa mpango kwa ushirikiano na viongozi wa kanisa mahalia kusanifu na kuboresha misioni ili iwe na matokeo yanayotarajiwa katika taifa la Ethiopia. Mpango huo ulidai kanisa libadilishe iliyokuwa union moja ya Ethiopia kuwa misioni za union mbili ambazo zingeweza kuwafikia watu wengi zaidi. Baada ya miaka minne ya kazi ngumu, hatimaye wamekidhi matakwa yote na vigezo vya kuanzisha union mbili zilizo imara katika taifa.

Aliyepewa jukumu la kuongoza jitihada hizi za kutayarisha utekelezaji huu ni Mchungaji Temesgen Bulti aliyekuwa Mwenyekiti wa Union Misioni ya Ethiopia hapo awali. Anasema kwamba matumaini "kuwa matokeo ya kugawanya iliyokuwa union ya Ethiopia kuwa mbili yataleta ukuaji wa ajabu katika Misioni ya Mungu ya Ethiopia. Nchi ya Ethopia ni kubwa na ina wakazi zaidi ya milioni 110. Zoezi la kusogeza huduma kwa jumuia mahalia litafungua fursa ambazo zisingeweza kufikiwa hapo kabla. Union mbili hizi mpya zikiwa na himaya ndogo kuliko ilivyokuwa union moja hapo kabla, zina fursa ya ajabu ya kujikita katika maeneo ambayo hayajafikiwa."

Misioni ya Waadventista kule Ethiopia sasa imepangwa kuwa Misioni ya Union ya Magharibi mwa Ethiopia na Misioni ya Union ya Mashariki mwa Ethiopia. Kulingana na sera za kanisa, ile iliyokuwa Union ya awali, yaani Misioni ya Union ya Ethiopia ilivunjwa ili kuwezesha hizo union mbili kufanyika, na kamati kuu ilipitisha uchaguzi wa uongozi katika hizo union mbili kulingana na sera. Divisheni ya ECD inamkaribisha Geremew Biru, Belay Taye na Chali Birasa kama Mwenyekti, Katibu mtendaji, na Mhazini wa Mision ya Union ya Magharibi mwa Ethiopia, na Tadesse Adugna, Petros Negash na Chali Birasa kama Mwenyekiti, Katibu mtendaji, na Mhazini wa Misioni ya Union ya Mashariki mwa Ethiopia.

ECD imefanya kitengo cha mahusiano ya Waislamu na Waadventista (AMR) kuwa ndicho kipaumbele kote katika divisheni, na inatazamia kutoa uongozi katika jumuia ya Waadventista wa Sabato kote ulimwenguni katika eneo hili la huduma. Ethiopia ni eneo mkakati la huduma kwa misioni ya Waadventista hususan katika suala hili kwa sababu kuna mivuto mikubwa ya wakazi wengi walio Waislam na kwa hiyo kuwa fursa kubwa kwa kutokea kwa misioni ya Waadventista. Karibia asilimia 80 ya taifa hilo ni Waislam au Wa-Orthodox. Wengi hawatambui kwamba Pastor Temesgen Bulti, aliyekuwa Mwenyekiti wa Misioni ya Union ya Ethiopia anatambuliwa kama mmoja wa mamlaka ya kanisa la Waadventista wa Sabato inayoongoza katika Uislam na Ukristo. Yeye ni mtarajiwa wa shahada ya uzamivu katika eneo la uhusiano wa Waislam na Waadventista (AMR) na anatambuliwa na mkurugenzi wa mahusiano ya Waislam na Waadventista (AMR) Petras Banda kama mmoja wa washauri wakuu katika huduma hiyo. Kwa kuwa Uislam ni dini yenye mvuto mkubwa ndani ya Ethiopia, Mchungaji Bulti sasa ameombwa kuongoza huduma hii ya AMR, na huduma kwa Imani ya Wa-Orthodox na kuongoza idhaa mpya ya saa 24 ya Hope Channe Ethiopia katika Misioni ya Union ya Mashariki mwa Ethiopia.

Ethiopia ilikuwa ni nchi lengwa kwa mahubiri ya Kuwahusisha Wahiriki Wote (TMI) yaliyofanyika kote katika divisheni mwaka 2019 ambapo watu zaidi ya 25,000 walibatizwa na kuwa washiriki wapya. Ushirika wa Waadventista wa Sabato na jumuia za Ethiopia wametiwa nguvu na mahubiri ya uinjilisti na wanaendeleza uinjilisti wakiwa na ari mpya. Union za ECD zinaendelea pia kuwekeza katika misioni katika Ethiopia kwa kufadhili wamisionari wanaoshiriki injili katika maeneo ambayo hayajafikiwa. Washiriki wote wanahimizwa kuombea union mbili hizi mpya, uongozi wake na ari mpya ya kuwafikia kwa idhaa ya hope (hope channel), watu wa Imani ya Uislamu, na Wa-Orthodox ndani ya Ethiopia. Mchungaji Bulti anashiriki kwamba "angependa kuwashukuru washiriki wa kanisa ndani ya Ethiopia na nje ya nchi kwa mshikamano waliouonesha katika zoezi la kugawanya union wakiwa na mtazamo wa kimisioni. Jambo hili lilifanyika kwa roho ya uzuri. Ninamsifu Bwana, watendakazi wenzangu, ngazi za juu za kanisa, Waadventista waliosambaa duniani, na washiriki wa kanisa letu."

Mchungaji Emanuel Pelote ni Mhariri wa Gazeti la "Connect" na Msaidizi wa Rais wa Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati

Mkutano wa Vijana Hai waleta Msukumo 350 Ndani ya Arusha



Chuo kikuu cha Arusha katika Union Konference ya Kaskazini mwa Tanzania (NTUC) kilikuwa mwenyeji wa mkutano wa mafunzo ya Vijana Hai ngazi ya divishehi kuanzia tarehe 2 hadi 7 Desemba 2019. Huu ulikuwa ni mkutano wa kwanza wa aina yake ndani ya divisheni ukiwa na wawezeshaji kutoka Halmashauri Kuu ya kanisa la Waadventista wa Sabato na kutoka makao makuu ya Divisheni ya Afrika Mashariki na Kati. Vijana takribani 350 walihudhuria kutoka Tanzania, Kenya na Rwanda ambao tunatarajia kwamba watakuwa viongozi katika makanisa yao mahalia na hivyo watashiriki mibaraka waliyopata katika mkutano huo.

Vijana Hai ni program ya uanafunzi wa vijana iliyosanifiwa kujenga hali ya kurejea kwa vijana waliopevuka na walio wazima kwa kuwatia moyo na kuwasheheneza namna ya kufanya chaguzi za mtindo wa maisha wenye afya. Mkutano huo ulikusudia kutia moyo vijana kukubali kipawa cha Mungu cha wokovu na changamoto yake ya kuishi kwa kuwatumikia wengine na kutumia vipawa vya pekee katika kutimiza utume wa Mungu.

Daktari Fesaha Tsegaye ni mkurugenzi wa Huduma za Afya katika ECD na mratibu wa mafunzo na mikutano ya Vijana Hai ya ECD

Shilingi za Kenya Milioni 15 zimechangwa kwa ajili ya sehemu za makazi za wafanyakazi wa field ya Ziwa Victoria



Mheshimiwa Daktari Fred Matiangi pamoja na kuwa mfanyakazi wa serikali ya Kenya katika ngazi za juu sana anatumika pia kama Katibu wa Bunge kwa Uratibu wa Ndani. Lakini pia ni mshiriki wa kanisa la Waadventista wa Sabato aliyejitoa kwa dhati. Kwa kuonesha kwamba kuwahusisaha washiriki wote kunaweza kufanyika kwa namna nyingi, Daktari Matiangi aliongoza zoezi la kuchangia ujenzi wa nyumba za wafanyakazi tarehe 27 Oktoba 2019 ambao uliandaliwa na makao makuu ya field ya Ziwa Victoria ambapo waliweza kuchanga shilingi za Kenya milioni 15.

Kusudi la kuchangia ni kutegemeza ujenzi wa nyumba za viongozi wa field ya Ziwa Victoria iliyoanzishwa miaka mitatu iliyopita. Kwa miaka mitatu hiyo, viongozi walitambua kwamba kujenga nyumba nane zenye gorofa kwa ajili ya viongozi wa idara kungepunguza gharama kuliko kuendelea kulipa kodi ya pango kwenye nyumba za kupanga. Mchungaji Samson Okwach, ambaye ni Mwenyekiti wa hiyo Field aliwahakikishia wafadhili kwamba fedha hizo zingeelekezwa sehemu stahiki kwa matumizi ambayo yamekusudiwa na kuwahakikishia kwamba wangewajibika kwa kila senti itakayotumika.

Daktari Matiangi alisisitiza hitaji la umoja kwa viongozi wa kanisa na kuzungumza kwa sauti moja ili miradi ya maendeleo itekelezwe kwa Amani. Akihubiri wakati wa tukio hilo, Mchungaji Samwel Misiani, ambaye ni Mwenyekiti wa Konferensi ya Union ya Magharibi mwa Kenya alisisitiza katika neema ya Mungu kwa namna ilivyojidhihirisha katika Yohana 3:16-17. Aliwataka waumini kutembea kwa namna inayostahili wito wao.

Philip Gai ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Konferensi ya Union ya Magharibi mwa Kenya



Chuo Kikuu cha Bugema Chaadhimisha Miaka 25 Kwenye Mahafali

Mwezi wa Novemba mwaka 2019 chuo kikuu cha Bugema kilishuhudia maadhimisho ya miaka 25 kwa mahafali ya wanafunzi 1,518 wakitumia kaulimbiu isemayo *"Njozi zageuka kuwa halisi."* Wanafunzi wanaotoka katika nchi zaidi ya 20 walihitimu kutoka katika chuo kikuu cha Uganda. Pamoja na hao wengi waliopata shahada yao ya kwanza, karibu asilimia 10 ya wahitimu walipata shahada ya uzamili na wengine asilimia kama 30 hivi walipata stashahada na vyeti. Shule inazidi kuvutia wanawake wangi ambao wanathamini elimu kama inavyooneshwa kwa asilimia 30 ya wahitimu wakiwa ni jinsia ya kike.

Mzungumzaji aliyeanza alikuwa ni Profesa Mary J. N. Okwakol ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Baraza la Taifa la Elimu ya Juu Uganda. Baada ya kukipongeza chuo kikuu kwa kuafikiana na viwango vya Baraza la Taifa la Elimu ya Juu, mgeni rasmi aliunga mkono suala la kuhusisha shule za msingi pamoja na halmashauri ya eneo mahalia katika sherehe za kuhitimu. Alisema kwamba hii ilikuwa ni mara ya kwanza kwake kushuhudia kuhusishwa kwa namna ya pekee kwa jumuia katika mpangilio wa mahafali ya chuo kikuu.

Ushauri wa mzungumzaji kwa wahitimu ni kwamba katika kila jambo wanalofanya watangulize shauku zao wasitangulize pesa. Aliwahimiza kutambua njozi zao, kwamba ziwe na taswira sahihi ya kile wanachotaka kupata na kuendelea kutafuta sifa stahiki, stadi, na ujuzi unaotakiwa ili kufikia njozi hizo. Ushauri wake ulisisitiza umuhimu wa kuwa na malengo na mipango mahususi, wakifanyia kazi kwa mpangilio na maamuzi pia wakifanyia kazi malengo yao kwa dhati na kujitoa kikamilifu.

Profesa Okwakol pia aliwatahadharisha kwamba wanaweza wakakatishwa tamaa katika njia hiyo na watu au mazingira ambayo yanatishia kutimizwa kwa njozi zao. Hata hivyo aliwashauri kwamba huo ndio wakati wa kukumbuka kubakia katika malengo na mipango ya mtu, huku ukipuuza mivuto hasi. Aliwaonya pia wahitimu dhidi ya kupanga huku wakijenga katika kupanga wakilenga kutajirika haraka. Badala yake, aliwahimiza kuweka malengo halisi ya fedha na kuyafanyia kazi kwa uvumilivu na kujitoa kikamilifu.

Mwanzo wa hotuba yake alikuwa na neno la ushauri kwa wazazi pia. Walihimizwa kuendelea kuongoza watoto wao kadiri ambavyo hekima yao ingeendelea kuwa ya thamani hata baada ya wanafunzi wao kuhitimu.
Mkuu wa Chuo Kikuu, Daktari Daniel Matte alishauri wahitimu kutumia kwa ukamilifu talanta zao na kuzikuza katika fani zao. Aliwahimiza wahitimu kutafuta namna ya kuwekeza uwezo wao katika nchi za nyumbani badala ya kutafuta fursa nchi za nje. Mkuu wa Chuo Kikuu huyo aliwapa changamoto "kufanya maeneo yao ya kazi yawe ni malisho ya kijani ili wasiende kutafuta malisho yanayoonekana kama kijani kwingine." Aligusia kwamba, sekta binafsi ni kiini cha maendeleo na ni uwanja unaotengeneza ajira, Daktari Matte aliongeza kwamba ikiwa kwa hakika umuhimu ndiyo kama mama wa uvumbuzi, basi Afrika inatakiwa kuongoza katika uvumbuzi na ubunifu.

Makamu wa Mkuu wa Chuo Profesa Patrick Manu aliwashukuru watu wote waliohudhuria kwenye tukio hilo na kuahidi kuendelea kuongoza Chuo Kikuu cha Bugema katika viwango vya juu. Aliwatunuku watu kadhaa kwa utumishi wao uliotukuka kwa chuo kikuu.

Immanuel Ogwal ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Misioni ya Union ya Uganda







AUCA Wanasherehekea Maendeleo katika Sherehe ya Mahafali ya 25

Jumapili ya tarehe 25 November 2019, darasa la kwanza la wanafunzi wa uuguzi lilihitimu ngazi ya Shahada ya kwanza kutoka katika Chuo Kikuu cha Afrika ya Kati (AUCA) pamoja na wengine takriban 627 waliofuzu katika ngazi hiyo hiyo na program ya shahada ya uzamili. Sherehe za mahafali zilifanyika kwa mara ya 25 katika chuo hicho ngazi ya shahada, na mara ya tatu kwa ngazi ya shahada ya uzamili. Shule hiyo ilishuhudia wanafunzi 307 wakifuzu ngazi ya shahada ya kwanza ya Uongozi masuala ya Biashara, na 65 shahada ya uzamili katika kitivo cha uongozi wa Biashara. Pamoja na hao, kulikuwa pia na wahitimu 162 katika Teknohama, 45 katika Uuguzi, 18 katika Teolojia, na 8 shahada ya uzamili katika elimu, na hatimaye 67 waliohitimu katika shahada ya kwanza katika elimu.

Chuo Kikuu hicho pamoja na wanachuo wote wanayo sababu ya kujivunia jitihada zao. Wahitimu 347 kati ya wahitimu 672, walifanya vizuri sana na kupata daraja la kwanza katika utendaji wao kimasomo. Hii inaonesha ubora wa juu sana wa elimu katika chuo hicho. Ngazi ya matokeo pia inashuhudia ile roho ya bidii ambayo wahitimu wameonesha wakati chuo kikuu hicho kikifundisha kule AUCA.

Daktari Hesron Byilingiro, ambaye ni Mwenyekiti wa Misioni ya Union ya Rwanda ya kanisa la Waadventista wa Sabato aliwahutubia wahitimu akiwasisitiza “kuoanisha stadi zao na mahitaji ya jumuia ili kugusa maendeleo ya uchumi wa jamii katika nchi kwa ujumla. Hao wahitimu wakiitikia wito huo waliahidi kutumia stadi walizopata na elimu kutoka AUCA kama njia ya kurudisha kwenye jumuia. Akiakisi hitaji la kunufaisha jumuia, makamu wa Mkuu wa Chuo wa AUCA, Daktari Roger Ruterahagusha alisisitiza kwamba Chuo Kikuu kiko makini kuchangia kwenye sekta ya Afya ya Rwanda kwa kuzalisha Wauguzi wenye sifa stahiki na shindani.

Ng’ambo ya program hii ya uuguzi, Divisheni ya Waadventista wa Sabato ya Afrika Mashariki na Kati (ECD) inaanzisha sasa hivi kitivo cha tiba katika chuo kikuu cha AUCA ikilenga katika kugusa jumuia kwa namna iliyo chanya kote katika jimbo la Afrika Mashariki na Kati hata ng’ambo ya mipaka yake. Kitivo hicho kinafanya matayarisho kuanza mafunzo mapema mwaka 2020 katika eneo la kitivo cha AUCA cha Masoro. Shule ya kisasa ya tiba itawezesha wanafunzi ambao wametoka maeneo yote ya jimbo la Afrika Mashariki na Kati, ili kuwezesha huduma ya tiba ya viwango vya kimataifa, huduma ya Afya na uongozi katika sekta ya afya kwa watu mmoja mmoja, jumuia na hata taifa kwa ujumla.

Daktari Blasious Ruguri ambaye ndiye Mkuu wa Chuo Kikuu cha AUCA na Mwenyekiti wa ECD, aliwapa changamoto wahitimu kufikiria kwa mapana na kuwa na mivuto ya kimataifa kwa sababu ni faida kuhitimu kutoka katika Chuo Kikuu chenye hadhi ya kimataifa kama AUCA.

Ferdinand Mbonaruza ni
Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano
wa Chuo Kikuu cha Afrika ya Kati (AUCA)



Umri Siyo Suala Katika Kufanya Uamuzi wa Kumfuata Yesu Kristo

Hata kama kuzaliwa kwao upya katika maji ya ubatizo kumewafanya kuonekana wachanga katika Imani ndani ya kanisa la Waadventista wa Sabato la Alo kule Kusini Mashariki mwa Field ya Ethiopia, bado wao pia wamo kati ya wakongwe wa Imani. Ndugu wawili kwa majina, Kaka Buli Karbamo Tosi mwenye umri wa miaka 96, na Dada Ligo Koji Foge mwenye umri wa miaka 96 walibatizwa siku ya Ijumaa, tarehe 22 Novemba 2019 katika maji ya uvuguvugu katika chemchemi ya mlima Wondo Genet yenye maji ya moto. Kanisa hilo ambalo liko hai lilikuwa na ratiba ya ubatizo kwa walengwa kadhaa siku ya Sabato tarehe 23 Novemba, lakini wakaamua kuwabatiza hawa wakongwe walioamini siku moja kabla ya siku iliyopangwa katika eneo ambalo lingekuwa salama zaidi kwao kufika kwa kutembea. Mto ambao ungetumika kwa ubatizo wa wengine ulihitaji kupanda milima na mabonde kabla hawajafika.

Hawa ndugu wawili ambao hawakuruhusu ugumu wa kufika mahali pa kubatizia usababishe kuahirisha kujitoa kwao kwa Kristo, wamekuwa wakijifunza masomo ya Biblia kwa takribani mwaka mmoja sasa. Ligo alikuwa na uelewa wa kanisa la Waadventista wa Sabato na mafundisho yake kwa muda mrefu. Hata kama hakuwa na shauku kwa kanisa, bado alijisikia kuwa mazingira yake hayakuwa mazuri kiasi kwa yeye kufanya maamuzi hadi sasa. Kwa upande mwingine, Buli hakuwahi kusikia kuhusu ujumbe wa Waadventista kabla ya mwaka huo. Wakati ulipokuwa muafaka, Mungu alimtuma Medso Tufa Koji, ambaye ni mpwa wao kuwatembelea na kuombea, ombi lililosababisha wakabatizwa.

Kwa kweli ni lazima tuendelee kuomba kwamba Bwana wa mavuno atume watendakazi katika shamba lake kwa sababu mavuno ni mengi na yamekomaa!

Kwa kweli ni lazima tuendelee kuomba kwamba Bwana wa mavuno atume watendakazi katika shamba lake kwa sababu mavuno ni mengi na yamekomaa!

Mungu waliwapa hawa washiriki wawili wapya fursa yao ya kwanza kushuhudia utukufu wake katika maji ya ubatizo. Baadhi ya washiriki wa jumuia ambao hawakuwa kati ya Waadventista waliokuwa wanasherehekea ubatizo, waliamua kushiriki katika mazingira haya ya kiroho wakisema: “Hebu tufurahie kuogelea katika haya maji matakatifu ambayo yamebarikiwa kwa maombi.” Jina lake liendelee kubarikiwa na kutukuzwa.

Kisa na **Athanase Rutebuka**, Chuo cha Waadventsta wa Sabato cha Ethiopia. **Medaso Tufa Koji** na **Tesfaye Bekele Dello** walichangia katika kisa hiki.





Konferensi ya Union ya Kenya Magharibi Wakipeleka Zoezi la Kuhusisha Washiriki Wote (TMI) kwenye Mizizi

Mwezi wa nane mwaka 2019, Konferensi ya Union ya Kenya Magharibi ilielekeza utume wa kuhusisha washiriki wote (TMI) katika maeneo 94 tofauti ndani ya Konferensi ya Bonde la Ufa (GRVC). Mwisho wa kipindi cha majuma mawili ya mavuno, roho 98 zilibatizwa na mbegu nyingi zikawa zimepandwa katika mioyo ya watu ambao walikuwa wameingia katika safari ya kutoa maisha yao kwa Bwana. Mwisho wa kila kitu, makanisa saba yalijengwa.

Kule Kapkitony, ambapo Mchungaji Ochorokodi anahudumu, mshiriki mmoja wa Waadventista wa Sabato mwenye ukarimu alichangia kwa kutoa ardhi yake, na kanisa likajengwa mara moja. Familia yote ya huyo mshiriki mkarimu baada ya tukio hilo walibatizwa wote.

200

Wahubiri waliokuwemo wakiwa wametawanyika kote katika jitihada za pamoja za utume wa kuhusisha washiriki wote (TMI)

Daktari Martin Akoto aliongoza huduma ya huruma na nyumba ilijengwa na washiriki wa kanisa ili kuhifadhi mtu aliyekuwa mhitaji. Kitendo hiki cha upendo kilisababisha roho nyingi katika eneo hilo kumgeukia Kristo, na kati ya hao baadhi yao walibatizwa.


Mchungaji Roselyne Ayayo alihudumu kule Underit ambapo watu 28 ambao hapo awali walikuwa walevi walibatizwa. Watu hao sasa wameunda kwaya na wanahudumia rafiki zao. Mchungaji huyo ameanza program ya kufuatilia, na roho nyingi sasa zinajiunga katika kundi.

Mzee Daniel Tirop alichanganya huduma ya kuhubiri na huduma ya afya katika Kapwosor na matokeo kwa kweli yalikuwa ya ajabu sana. Jengo kubwa la kudumu linajengwa katika eneo lile lile ambao maisha ya wengi yanaelekezwa kwa Yesu kila siku.

Kulikuwa na zaidi ya wahubiri 200 wakiwa wametawanyika kote katika himaya ya Konferensi ya Bonde la Ufa (GRVC). Wahubiri ambao ni Wachungaji na Walei walifanya kazi pamoja katika jitihada za pamoja. Kwaya nyingi na vikundi vya vijana walitegemeza hawa wahubiri kwa jitihada zao binafsi.

Kulikuwa na mvua kubwa, baridi na pepo kali zilizosababisha hali ya hewa kuwa mbaya sana, hata hivyo hilo halikuzuia wanaume na wanawake wa Mungu ambao walikuwa wamejitoa kikamilifu katika kueneza injili. Leo hii tunatabasamu kadiri tunavyorudi na kuona nyuma kile ambacho Bwana anatutendea katika sehemu za mizizi na ndani ya vijiji kama matokeo ya kuhusisha washiriki wote (TMI). Mungu atukuzwe kwa upeo wa juu.

Philip Gai ni Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Konferensi ya Union ya Kenya Magharibi



ADRA

EVERY CHILD.
EVERYWHERE.
IN SCHOOL.

Out-of-School Children

No child should ever be denied an education. Not because of where they live. Not because their government is failing to provide adequate and free education. Not because their family is poor. Not because of conflict or displacement. Not because of their gender, ethnicity, or disability. Every child, everywhere, has the right to attend school and get an education. Unfortunately, 262 million children, adolescents, and youth are currently denied this right.

A child who is out of school is more vulnerable to human traffickers and recruitment by militias, and at increased risk of early marriage, teen pregnancy, and child labor. An uneducated adult lacks the ability to lift themselves out of poverty, and their children face barriers at every stage of life: an increased risk of dying in infancy, malnourishment which affects their mental and physical development, and the continued cycle of poverty, dooming another generation.

Without education, nothing changes.
Disadvantage lingers.
Poverty continues.

SIGN THE PETITION
ADRA.org/InSchool

THE ADVENTIST DEVELOPMENT AND RELIEF AGENCY (ADRA) IS THE GLOBAL HUMANITARIAN ORGANIZATION OF THE SEVENTH-DAY ADVENTIST CHURCH.